JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2020

## KISWAHILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2020

# 01 KISWAHILI

*Kimechapishwa na*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2021

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ........................................ iv

1.0 UTANGULIZI ........................................ 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI ........................................ 2

2.1 Sehemu A: ........................................ 2
2.2 Sehemu B: ........................................ 8
2.3 Sehemu C: ........................................ 13
2.4 Sehemu D: ........................................ 18
2.5 Sehemu E: ........................................ 22

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI ........................................ 29

4.0 HITIMISHO ........................................ 30

5.0 MAPENDEKEZO ........................................ 31

KIAMBATISHO A ........................................ 33

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya wanafunzi waliofanya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa somo la Kiswahili mwaka 2020. Taarifa hii inachambua majibu ya maswali husika kwa lengo la kutoa mrejesho kwa walimu, wanafunzi, watunga sera, wathibiti ubora wa Shule, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu. Vilevile, taarifa hii imebainisha jinsi mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ulivyomsaidia au kutomsaidia mwanafunzi kupata maarifa stahiki kwa kipindi cha miaka miwili ya elimu ya Darasa la (iii) na (iv).

Aidha, taarifa hii imeonesha changamoto mbalimbali zilizosababisha baadhi ya wanafunzi kushindwa kujibu maswali kwa ufasaha. Changamoto hizo ni; kushindwa kuelewa na kuchambua mawazo yaliyowasilishwa katika kifungu cha habari, uwepo wa athari ya lugha mama, kushindwa kumudu stadi za kusoma na kuandika. Pia, kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana za nahau pamoja na kukamilisha methali mbalimbali. Aidha, wanafunzi walishindwa kupanga sentensi katika mtiririko unaoleta mantiki.

Hata hivyo, umahiri wa mwanafunzi umepimwa kwa kuzingatia viwango vinne vya ufaulu ambavyo ni; kiwango hafifu, cha wastani, kizuri na kiwango kizuri sana. Mtawanyiko wa majibu ya wanafunzi kwa kila swali umeainishwa katika uchambuzi huu kwa kutumia vielelezo, chati na maelezo. Kwa ujumla ufaulu wa wanafunzi ulikuwa mzuri kwani asilimia **90.09** walifaulu Upimaji wa somo la Kiswahili.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa, taarifa hii itawasaidia wanafunzi na wasimamizi wa elimu kuchukua hatua stahiki ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa lengo la kutatua changamoto zilizoainishwa katika taarifa hii. Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania linaamini kuwa, maoni yaliyotolewa yakifanyiwa kazi, yataongeza umahiri wa wanafunzi na kuimarisha ubora wa elimu inayotolewa nchini.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki kuandaa taarifa hii wakiwemo Maafisa Mitihani.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho wa namna wanafunzi walivyojibu maswali ya Upimaji wa somo la Kiswahili mwezi Novemba 2020. Upimaji huu ni wa tatu katika mtaala mpya unaozingatia ujenzi wa umahiri kwa mwanafunzi katika stadi za kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika.

Umahiri uliopimwa katika somo la Kiswahili zilikuwa tano, ambazo ni; *Uwezo wa mwanafunzi katika kusikiliza matamshi ya silabi, maneno na sentensi na kuyaandika* (*Imla*). Umahiri wa *kutambua nyakati mbalimbali, umahiri wa kutoa maana ya nahau na kukamilisha methali mbalimbali*, umahiri wa *kupanga sentensi katika mtiririko unaoleta maana,* pamoja na umahiri *wa kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika habari*. Sehemu hizo tano zimetoka katika umahiri mkuu ambao ni *Kuwasiliana Katika Miktadha Mbalimbali* na *Kuonesha Uelewa wa Jambo Alilolisikiliza au Kulisoma*. Kila sehemu ilikuwa na swali **moja** (**1**) lenye vipengele **vitano** (**5**) vyenye jumla ya alama kumi (10).

Jumla ya wanafunzi **1,828,265** walisajiliwa kufanya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne mwaka 2020 na waliopimwa katika somo la Kiswahili walikuwa **1,702,918**. Aidha, wanafunzi **1,534,049** sawa na asilimia **90.09** ndio waliofaulu katika upimaji huo. Hata hivyo, kumekuwa na ongezeko la ufaulu kwa asilimia 2.23 kutoka (88.67%) mwaka 2019 hadi (90.09%) mwaka 2020 katika somo la Kiswahili. Viwango vya ufaulu katika majibu ya wanafunzi vimegawanyika katika sehemu nne kulingana na alama walizopata ambazo kiwango hafifu ni 0-2.5, wastani 3-6, mzuri 6.5 -9.5 na kizuri sana ni alama 10.

Wanafunzi waliopata wastani, kiwango kizuri na kizuri sana ndio waliohesabika kuwa wameweza kujibu maswali kwa usahihi. Hata hivyo, waliopata kiwango hafifu wamehesabika kushindwa kujibu maswali kwa usahihi.

Aidha, katika taarifa hii, uchambuzi wa takwimu umewasilishwa kwa njia ya chati. Rangi mbalimbali zimetumika kuonesha viwango vya ufaulu na asilimia ya wanafunzi kwa kila swali ambapo rangi nyekundu imetumika kiwango hafifu cha ufaulu, yaani **0 – 33,** rangi ya njano imetumika kuwakilisha kiwango cha wastani, yaani asilimia **34 – 66**, rangi ya kijani mpauko na kijani iliyoiva zimetumika kuwakilisha kiwango kizuri na kizuri sana mtawalia yaani asilimia **67 – 100**.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI

Sehemu hii inaainisha maswali yote yaliyoulizwa na majibu ya wanafunzi kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa kwa kila sehemu. Idadi na asilimia ya wanafunzi waliojibu vizuri na walioshindwa kujibu vizuri vimeoneshwa katika chati. Hata hivyo, taarifa hii imeonesha sababu za ufaulu na kutofaulu kwa mwanafunzi kwa kila swali. Sampuli za majibu hafifu, wastani na mazuri zimetumika kuonesha viwango vya ufaulu kwa baadhi ya wanafunzi katika maswali.

### 2.1 Sehemu A:

Sehemu hii ilikuwa na swali moja la imla ambapo mwanafunzi alitakiwa kusikiliza kwa makini sentensi tano (05) alizosomewa kisha kuziandika kwa usahihi. Kila sentensi ilikuwa na maneno manne yenye alama nusu ($00^1/_2$) kwa kila neno. Kila sentensi ilikuwa na alama 2, hivyo kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama (10). Swali lilitoka kwenye umahiri mkuu wa *Kuwasiliana katika Miktatha Mbalimbali*.

Swali lililenga kupima uelewa wa mwanafunzi katika kuandika sentensi kwa kuzingatia alama za uandishi na kutambua sauti mbalimbali katika matamshi ya silabi, maneno na sentensi.

**Swali la 1**:**Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) ____________________________________________

(ii) ____________________________________________

(iii) ____________________________________________

(iv) ____________________________________________


(v) ____________________________________________

Zifuatazo ni sentensi walizosomewa wanafunzi:

(i) Fikiri ni mpwa wangu.
(ii) Asante sana mwalimu wetu.
(iii) Baba anakunywa maji mengi.
(iv) Daktari alitushauri tutunze masikio.
(v) Thamani ya elimu imedhihirika.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,702,640 sawa na asilimia100. Kiwango cha ufaulu cha wanafunzi katika swali hili kilikuwa kizuri kwani wanafunzi 1,448,168 sawa na asilimia 85.1 walijibu vizuri swali hili. Wanafunzi 556,668 sawa na asilimia 32.69 waliweza kujibu vizuri sana vipengele vyote 5 na kupata alama zote 10. Aidha, wanafunzi 733,943 sawa na asilimia 43.11 walifanya vizuri na kupata alama 6.5 hadi 9.5 kwani waliandika kwa usahihi maneno 13 - 19. Wanafunzi 157,557 sawa na asilimia 9.25 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6 ambapo waliweza kuandika maneno 6-12.

Wanafunzi 254,472 sawa na asilimia 14.95 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 2.5 kwa kuwa waliandika maneno 0-5 tu. **Chati Na. 1**. inaonesha viwango vya ufaulu vya wanafunzi kwa asilimia.




**Chati Na. 1:** *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 1*

Uchambuzi unaonesha kuwa, wanafunzi 556,668 sawa na asilimia 32.69 walifaulu kwa kiwango kizuri sana kwani waliweza kuandika maneno yote ishirini kwa usahihi. Wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kusoma na kuandika hivyo kuweza kubaini sauti zinazounda maneno yaliyosomwa kisha kuyaandika kwa usahihi huku wakizingatia alama za uandishi pamoja na kutumia herufi kubwa mwanzoni mwa sentensi.

Aidha, wanafunzi hao walikuwa na uelewa wa kubaini na kuandika silabi zenye herufi mwambatano kama vile maneno *mpwa* silabi *pwa*, *mwalimu* silabi *mwa*, *anakunywa* silabi *nywa*, *daktari* silabi *kta*, *thamani* silabi *tha* na *imedhihirika* silabi *dhi.* Maneno hayo ni miongoni mwa maneno yaliyounda sentensi za imla walizosomewa.

Kwa ujumla, wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kusikiliza na kubaini matamshi ya herufi zinazounda maneno pamoja na kuandika alama za uandishi kwa usahihi. Kielelezo Na. 2.1.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi vipengele vyote vitano (5) vya swali hili.

1. **Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) Fikiri ni mpwa wangu.
(ii) Asante sana mwalimu wetu.
(iii) Baba anakunywa maji mengi.
(iv) Daktari alitushauri tutunze masikio.
(v) Thamani ya elimu imedhihirika.

Kielelezo Na. 2.1.1: *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 1*

Kielelezo Na. 2.1.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi ambaye aliweza kuandika kwa usahihi sentensi zote tano kwa kuzingatia alama za uandishi hivyo kupata alama zote 10.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, wanafunzi 157,557 sawa na asilimia 9.25 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6 kwani waliweza kuandika kwa usahihi maneno 6 hadi 12 kati ya maneno 20 yaliyounda sentensi zote tano. Wanafunzi hao, walikuwa na maarifa ya matumizi ya alama za uandishi ingawa walishindwa kuandika baadhi ya maneno yenye silabi mwambatano. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alichanganya matamshi ya herufi *l* na *r* kwenye neno “fikiri” na neno “alishauri” na kuandika “fikili”, na “alishauli”. Pia alishindwa kutofautisha kati ya sauti *th* na *s* kwa kuandika neno “samani” badala ya “thamani”.

Vilevile, alichanganya herufi kubwa na ndogo kwenye maneno aliyoyaandika kama vile, neno "mpwa" katika kipengele cha (i) aliandika "mPwa", neno "alitushauri" katika kipengele (iv) aliandika "alituShauli". Aidha, aliunganisha baadhi ya maneno katika kipengele (i) na (iii). Kielelezo Na. 2.1.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani.

1. **Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) fikilinimPwa wangu

(ii) ASante Sana mwalimu wetu

(iii) Baba anakunyamajimengi

(iv) Dakitali alituShauli kutunze masikio


(v) Samani ya elimu imidhihilika

Kielelezo Na. 2.2.2: *Sampuli ya jibu la wastani katika swali la 2*

Kielelezo Na. 2.2.2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeweza kuandika baadhi ya maneno kwa usahihi na kushindwa kuandika maneno yenye silabi mwambatano pamoja na kutozingatia kanuni za uandishi, hivyo kupata alama za wastani.

Hata hivyo, wanafunzi 254,472 sawa na asilimia 14.95 walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwani walishindwa kuandika kwa usahihi maneno waliyosomewa. Wanafunzi wengine walishindwa kuandika neno hata moja katika sentensi zote, hivyo kupata alama kuanzia 0 hadi 2.5. Wanafunzi hao walishindwa kuandika kwa usahihi sauti za herufi za silabi ambazo huunda maneno ili kuunda sentensi.

Aidha, baadhi yao hawakuwa na umahiri wa kusoma na kuandika, hivyo kushindwa kufuata misingi na taratibu za uandishi katika lugha ya Kiswahili, hasa katika miundo ya silabi katika kuunda neno. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alianza sentensi kwa herufi ndogo kwenye kipengele cha (ii) katika neno “asante”. Pia, aliandika maneno kwa herufi kubwa katikati ya sentensi katika kipengele cha (i) neno “Mubu” na (ii) “Mwalimu”. Aidha, alishindwa kuandika neno “mpwa” na kuandika “Mubu” katika kipengele cha (i). Vilevile, katika kipengele cha (ii) badala ya kuandika neno “Asante” aliandika “asate”. Hii inadhihirisha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na umahiri wa kusikiliza na kubaini matamshi ya herufi yanayounda maneno. Vilevile, walikosa umahiri katika alama za uandishi na walishindwa kuzingatia taratibu za uandishi, hivyo kuanza sentensi kwa herufi ndogo badala ya kubwa. Kielelezo Na. 2.1.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyetoa majibu yasiyo sahihi katika swali hili.


1. **Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi** katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) Fikiri ni Mubu wegu.

(ii) asate sana Mwalimu wetu.

(iii) Baba anatutu a maji megi'

(iv) Dakitri Alisauli tutuzi Masikio.

(v) Saman wafLimu amexgiliza.


Kielelezo Na. 2.1.3: *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 1*

Kielelezo Na. 2.1.3 kinaonesha majibu ya mwanafunzi ambaye alishindwa kuandika baadhi ya maneno kwa usahihi, pamoja na kuchanganya herufi kubwa na ndogo katika maneno yaliyounda sentensi kinyume na taratibu za uandishi katika Lugha ya Kiswahili.

## 2.2 Sehemu B:

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano ambavyo mwanafunzi alitakiwa kuchagua jibu sahihi kisha kuandika herufi ya jibu hilo katika kisanduku alichopewa.

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali*. Swali lilijibiwa na wanafunzi 1,702,640 sawa na asilimia 100. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani jumla ya wanafunzi 1,458,463 sawa na asilimia 85.70 waliweza kujibu vizuri. Wanafunzi 371,266 sawa na asilimia 21.81 walijibu vizuri sana vipengele vyote 5 na kupata alama 10. Aidha, wanafunzi 811,064 sawa na asilimia 25.09 walijibu vizuri na kupata alama 6.5 hadi 9.5. Wanafunzi 660,051 sawa na asilimia 38.77 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Vilevile, wanafunzi 244,177 sawa na asilimia 14.34 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 2.5. **Chati Na. 2.** inaonesha viwango vya ufaulu vya wanafunzi kwa asilimia.




**Chati Na. 2**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 2*

Vifuatavyo ni vipengele vya maswali ya kuchagua (i) - (v), ambapo mwanafunzi alitakiwa kuchagua jibu sahihi na kujaza katika kisanduku alichopewa.

(i) Neno "tumeimba" lipo katika hali gani?

A timilifu

B iliyopita

C iliyopo

D ijayo

Katika kipengele hiki wanafunzi waliweza kuchagua herufi A *timilifu* kuwa jibu sahihi. Wanafunzi hao walikuwa na ufahamu kuwa wakati timilifu huwakilishwa na kiambishi -me- kinachojitokeza katika kitenzi kwenye swali husika. Vilevile, walifahamu kuwa, wakati timilifu ni hali ambayo hutokana na kufanyika kwa kitendo muda mfupi uliopita. Hivyo, wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu nyakati mbalimbali za vitenzi.

Aidha, wanafunzi waliochagua kipotoshi B *ujao* walishindwa kuelewa kuwa wakati huo huwakilishwa na kiambishi -ta- katika kitenzi. Waliochagua kipotoshi C *uliopita* walishindwa kutofautisha kiambishi cha utokeaji wa wakati huo kuwa ni kiambishi cha -li- katika kitenzi na huelezea wakati uliopita ambao tendo lilitendeka. Pia, waliochagua kipotoshi D *uliopo* walishindwa kuelewa kuwa wakati huo huwakilishwa na kiambishi -na- katika kitenzi ambacho huelezea kuwa tendo linavyotendeka wakati huo huo.

(ii) Nilinunua matunda matamu. Neno "nilinunua" lipo katika wakati gani?

A Mtimilifu

B Ujao

C Uliopita

D Uliopo

Baadhi ya wanafunzi waliweza kuchagua herufi C *uliopita* kwani walikuwa na maarifa kuwa neno "nilinunua" lina kiambishi -li- ambacho huonesha tendo lilivyofanyika. Hivyo, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu nyakati mbalimbali za lugha ya Kiswahili, hasa wakati uliopita.

Hata hivyo, wanafunzi waliochagua kipotoshi A *timilifu* walishindwa kuelewa kuwa wakati huo huwakilishwa na kiambishi -me- katika kitenzi ambacho huonesha kuwa tendo limefanyika muda mfupi uliopita. Waliochagua herufi B *ujao* walishindwa kuelewa kuwa wakati huo huwakilishwa na kiambishi -ta- katika kitenzi na huonesha tendo litafanyika. Aidha, waliochagua kipotoshi D *uliopo* walishindwa kuelewa kuwa wakati uliopo huwa na kiambishi -na- katika kitenzi kinachoonesha kuwa kitendo kimefanyika wakati huo huo. Kwa ujumla, wanafunzi waliochagua vipotoshi hivyo hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu wakati uliopita, hususani kiambishi mahususi kinachowakilisha wakati uliopita katika kitenzi.

(iii) Watoto _____________ pilau juzi. Neno lipi kati ya maneno yafuatayo linakamilisha sentensi hii?

A watakula

B wanakula

C walikula

D hula

Katika kipengele hiki, baadhi ya wanafunzi waliweza kukamilisha sentensi kwa kuchagua herufi C *walikula.* Wanafunzi hao walikuwa na maarifa kuwa kitenzi “walikula” ndio jibu sahihi kwa sababu kina kiambishi -li- ambacho huonesha wakati uliopita. Aidha, wanafunzi hao waliweza kujua kuwa sentensi hiyo ipo katika wakati uliopita kutokana na neno “juzi” lenye maana ya siku iliyotangulia kabla ya jana. Neno hilo liliashiria kuwa kitendo hicho kilifanyika wakati uliopita kwa ujumla. Hivyo, wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya wakati uliopita.

Aidha, wanafunzi waliochagua kipotoshi A *watakula* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo lipo katika wakati ujao na huwakilishwa na kiambishi -ta- katika kitenzi ambacho huonesha tendo litakavyofanyika. Waliochagua kipotoshi B *wanakula* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo limeundwa na kiambishi -na- katika kitenzi na huonesha tendo la kula linavyofanyika. Pia, waliochagua kipotoshi D *hula* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo lina kiambishi hu- ambacho huonesha wakati wa mazoea katika utendekaji wa tendo (kula). Aidha, neno hilo haliwezi kukamilisha sentensi kwa kuwa sentensi husika ipo katika wakati uliopita. Hivyo, wanafunzi hao walikosa maarifa kuhusu dhana ya wakati uliopita na kushindwa kukamilisha sentensi husika kwa usahihi.

(iv) Neno lipi linaonesha wakati ujao kati ya maneno yafuatayo?

A Niliimba

B Nitaimba

C Huimba

D Ninaimba

Swali hili lilimtaka mwanafunzi kubainisha neno linaloonesha wakati ujao katika maneno aliyopewa na kuchagua herufi ya jibu sahihi. Katika kipengele hiki, wanafunzi waliweza kubainisha neno linaloonesha wakati ujao katika maneno waliyopewa kwa kuchagua

herufi B *nitaimba.* Wanafunzi hao walikuwa na maarifa kuwa neno "nitaimba" limeundwa na kiambishi -ta- ambacho huonesha wakati ujao, ambapo kitendo cha kuimba kitafanyika. Hivyo, wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya wakati ujao.

Pia, wanafunzi waliochagua kipotoshi A *niliimba* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo limeundwa na kiambishi -li- ambacho huonesha wakati uliopita. Waliochagua kipotoshi C *huimba* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo lipo katika wakati wa mazoea na huwa na kiambishi hu- ambacho mtenda hurejea tendo la kuimba mara kwa mara. Aidha, waliochagua kipotoshi D *ninaimba* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo halioneshi wakati ujao kwani limeundwa na kiambishi -na- kinachowakilisha wakati uliopo. Kwa ujumla, wanafunzi hao walikosa maarifa kuhusu dhana ya wakati ujao katika vitenzi.

(v) Mwalimu _______________ somo la Kiswahili sasa hivi.

A amefundisha

B alifundisha

C hufundisha

D anafundisha

Katika kipengele hiki wanafunzi waliweza kukamilisha sentensi kwa kuchagua herufi D *anafundisha*. Wanafunzi hao, walikuwa na maarifa kuwa neno "anafundisha" limeundwa na kiambishi -na- ambacho huonesha wakati uliopo katika kitenzi. Aidha, wanafunzi hao waliweza kujua kuwa sentensi hiyo ipo katika wakati uliopo kutokana na neno "sasa hivi" kwani linaonesha kuwa kitendo cha kufundisha kinafanyika muda huo. Hivyo, wanafunzi hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya wakati uliopo katika kukamilisha sentensi husika.

Hata hivyo, wanafunzi waliochagua kipotoshi A *amefundisha* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo lipo katika hali timilifu kwa kuwa

limeundwa na kiambishi -me- ambacho huonesha kuwa tendo limefanyika muda mchache uliopita. Waliochagua kipotoshi B *alifundisha* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo lipo katika wakati uliopita na huwa na kiambishi -li- ambacho huonesha wakati uliopita (alifundisha). Pia, waliochagua kipotoshi C *hufundisha* walishindwa kuelewa kuwa neno hilo lipo katika wakati wa mazoea ambapo huwa na kiambishi hu- ambacho huonesha kitendo kufanyika mara kwa mara. Kwa ujumla, wanafunzi hao walikosa maarifa ya kuelewa nyakati mbalimbali kutokana na kushindwa kufahamu viambishi mbalimbali vinavyowakilisha nyakati hizo katika vitenzi.

## 2.3 Sehemu C:

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5) na lilitoka katika umahiri wa *Kuonesha Uelewa wa Jambo Alilolisikiliza au Kulisoma*. Jumla ya alama katika swali hili zilikuwa 10 ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 02. Swali lililenga kupima umahiri wa mwanafunzi katika kutumia nahau na methali kwenye miktadha mbalimbali.

**Swali la 3:** (i) Toa maana ya nahau zifuatazo kwa kuandika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

(a) Kufa kishujaa______________________________

(b) Kifungua mimba____________________________


(c) Mkono wa birika ___________________________

(ii) Kamilisha methali zifuatazo kwa kuandika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

(a) Maji yakimwagika_____________________________


(b) Fuata nyuki__________________________________

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,702,640 sawa na asilimia 100. Kiwango cha ufaulu katika swali kilikuwa kizuri kwa sababu wanafunzi 1,185,308 sawa na asilimia 69.6 waliweza kujibu vizuri swali hili. Wanafunzi 56,786 sawa na asilimia 3.34 waliweza kujibu vizuri sana vipengele vyote 5 na kupata alama 10. Aidha, wanafunzi 497,558 sawa na asilimia 29.22 walifanya vizuri na kupata alama 6.5 hadi 9.5. Wanafunzi 630,964 sawa na asilimia 37.06 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Vilevile, wanafunzi 517,332 sawa na asilimia 30.38 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 2.5. **Chati Na. 3** inaonesha viwango vya ufaulu na asilimia ya wanafunzi.




Chati Na: 3: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 3*

Uchambuzi unaonesha kuwa, wanafunzi 56,786 sawa na asilimia 3.3 walikuwa na kiwango kizuri sana cha ufaulu na kupata alama 10, kwani waliweza kujibu vipengele vyote 5 vya swali kwa usahihi. Wanafunzi hao, waliweza kutoa maana sahihi ya nahau mbalimbali na kukamilisha methali kwa usahihi. Wanafunzi hao walikuwa na uelewa kuwa methali huundwa na pande mbili zinazotegemeana kidhima na kimaana. Mfano katika kipengele (i) (a) mwanafunzi alijibu kufa kishujaa ni *kufa kijasiri*, (i) (b) kifungua mimba ni *mtoto wa kwanza kuzaliwa*, (i) (c) mkono wa birika ni *kuwa mchoyo*. Vilevile, katika kipengele (ii) (a) maji yakimwagika *hayazoleki, na* (ii) (b) fuata nyuki *ule asali.* Hivyo, wanafunzi hao walikuwa na weledi na maarifa ya kutosha ya kueleza maana ya nahau na kukamilisha methali husika. Kielelezo Na. 2.3.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu vipengele vyote 5 vya swali kwa usahihi.


(i) Toa maana ya nahau zifuatazo kwa kuandika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

(a) Kufa kishujaa kufa kijasiri

(b) Kifungua mimba mtoto wa kwanza kuzaliwa.

(c) Mkono wa birika kuwa mchoyo.

(ii) Kamilisha methali zifuatazo kwa kuandika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

(a) Maji yakimwagika hayazoleki.


(b) Fuata nyuki ule asali.

Kielelezo Na. 2.3.1: *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 3*

Kielelezo Na. 2.3.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu vizuri kwa kufuata matakwa ya swali ambapo aliweza kutoa maana za

nahau katika vipengele vyote 3 na kukamilisha methali katika vipengele 2 kwa usahihi.

Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi 630,964 sawa na asilimia 37.06 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6 kwani waliweza kujibu vipengele 2 hadi 3 kwa usahihi. Baadhi yao walishindwa kutoa maana ya nahau katika vipengele na hawakuweza kukamilisha methali kwa usahihi. Kwa mfano, katika kipengele (i) (b) mwanafunzi alijibu “kifungua mimba ni *mtoto wa kwanza* (ii) (a) maji yakimwagika *hayazoleki* na (ii) (b) fuata nyuki *ule asali* na kushindwa kipengele (i) (a) kufa kishujaa *hakishindwi kutengenezekana* na (i) (c) mkono wa birika kuwa ni *mwizi.* Kielelezo Na. 2.3.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani.


(i) Toa maana ya nahau zifuatazo kwa kuandika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

(a) Kufa kishujaa hakishindwi kutengenezeka.

(b) Kifungua mimba mtoto wa kwanza.

(c) Mkono wa birika mwizi

(ii) Kamilisha methali zifuatazo kwa kuandika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

(a) Maji yakimwagika hayazoleki.


(b) Fuata nyuki ule asali

Kielelezo Na. 2.3.2: *Sampuli ya jibu la wastani katika swali la 3*

Kielelezo Na. 2.3.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa vipengele vingine kutokana na kushindwa kuelewa lugha ya picha iliyojengwa katika methali na nahau alizoulizwa.

Hata hivyo, wanafunzi 517,332 sawa na asilimia 30.38 walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu na kupata alama kuanzia 0 hadi 2.5. Baadhi yao walikuwa hawajui kusoma na kuandika na wengine hawakuwa na umahiri wa kutumia methali na nahau katika miktadha mbalimbali, hivyo kuandika maneno yasiyo na uhusiano na matakwa ya swali. Kwa mfano, katika kipengele cha (i) (a), mwanafunzi mmoja alitoa majibu ambayo sio sahihi kwa kuandika kufa kishujaa ni *zina uhakika ujao maneno,* (i) (b), kifungua mimba kuwa *ni ulanga watoto makini ujao*.

Aidha, katika kipengele (i) (c) mkono wa birika kuwa *hauvunjiki sana kuhusu ukataji* na kipengele (ii) (b) fuata nyuki kuwa *walijutia wanadamu.* Aidha, mwanafunzi huyo aliweza kutoa jibu sahihi katika (ii) (a) maji yakimwagika *hayazoleki*. Kwa ujumla, uchambuzi huu umebaini kuwa wanafunzi waliopata alama 0 na 2.5 walikosa maarifa kuhusu dhana ya nahau na methali na kutoelewa Lugha ya picha iliyotumika. Kielelezo Na. 2.3.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.


i) Toa maana ya nahau zifuatazo kwa kuandika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

(a) Kufa kishujaa zina uhakika ujao maneno

(b) Kifungua mimba ulanga watoto makini ujao

(c) Mkono wa birika hauvunjiki sana kuhusu ukataji

(ii) Kamilisha methali zifuatazo kwa kuandika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

(a) Maji yakimwagika haya zoleki

(b) Fuata nyuki walijutia wa nadamu

Kielelezo Na. 2.3.3: *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 3*

Kielelezo Na. 2.3.3 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu vibaya swali kwa kuandika maneno yasiyokuwa na uhusiano na matakwa ya swali kutokana na kutoelewa lugha ya picha iliyotumika katika nahau na methali katika swali husika. Aidha, aliweza kujibu kipengele (ii) (a) kwa sahihi.

## 2.4 Sehemu D:

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5) ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 2 na kufanya jumla ya alama 10. Swali lilitoka katika umahiri wa *Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali* na lililenga kupima ujuzi wa mwanafunzi wa kupanga mawazo katika mtiririko unaoleta mantiki.

**Swali la 4:** Sentensi zifuatazo zimechanganywa. Zipange katika mtiririko unaoleta maana kwa kuzipa herufi A, B, C, D na E. Sentensi ya (i) imetumika kama mfano.

(i) Nikifika shuleni ninaanza masomo. **F**

(ii) Kila siku ninaamka asubuhi. ______

(iii) Kisha ninaondoka kwenda shuleni.______


(iv) Ninapiga mswaki na kuoga. ______

(v) Dada ananipa chai na chapati. ______

(vi) Ninakunywa chai kwa chapati.______

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 1,702,640 sawa na asilimia 100. Wanafunzi 1,031,191 sawa na asilimia 60.6 walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu. Jumla ya wanafunzi 603,927 sawa na asilimia 35.47 waliweza kujibu vizuri sana vipengele vyote 5 na kupata alama 10. Aidha, wanafunzi 88,479 sawa na asilimia 5.20 walifanya vizuri na kupata alama 6.5 hadi 9.5.

Wanafunzi 338,785 sawa na asilimia 19.90 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Vilevile, wanafunzi 671,449 sawa na asilimia 39.44 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 2.5 **Chati Na. 4** inaonesha viwango vya ufaulu vya wanafunzi kwa asilimia.




**Chati Na. 4**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 4*

Uchambuzi unaonesha kuwa, wanafunzi 603,927 sawa na asilimia 35.47 walifaulu kwa kiwango kizuri sana kwani walijibu kwa usahihi vipengele vyote 5 na kupata alama 10. Wanafunzi hao, waliweza kupanga sentensi katika mtiririko unaoleta maana na kuandika herufi sahihi (ii) A (iii) E (iv) B (v) C na (vi) D. Hii inaonesha kuwa wanafunzi hao walikuwa na uwezo wa kubaini mtiririko wa matukio. Aidha, waliweza kubaini ni tukio gani limeanza na lipi limefuata kutokana na maana za sentensi husika. Kielelezo Na. 2.4.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu vipengele vyote 5 vya swali kwa usahihi.

4. Sentensi zifuatazo zimechanganywa. Zipange katika mtiririko unaoleta maana kwa kuzipa herufi A, B, C, D na E. Sentensi ya (i) imetumika kama mfano.

(i) Nikifika shuleni ninaanza masomo. **E**

(ii) Kila siku ninaamka asubuhi. A

(iii) Kisha ninaondoka kwenda shuleni. E

(iv) Ninapiga mswaki na kuoga. B

(v) Dada ananipa chai na chapati. C

(vi) Ninakunywa chai kwa chapati. D

Kielelezo Na. 2.4.1: *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 4*

Kielelezo Na. 2.4.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi kwa kuweza kupanga sentensi katika mtirirko unaoleta maana na kuunda kifungu cha habari.

Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 338,785 sawa na asilimia 19.90 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Wanafunzi hao waliweza kujibu vipengele 2 hadi 3 kwa usahihi kwani walikuwa na maarifa ya wastani ya kupanga sentensi katika mtiririko unaoleta maana. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alijibu kwa usahihi kipengele (ii) *A*, kwa kuelewa kuwa ndio sentensi inayoanza kwa sababu huelezea tukio ambalo kila siku analifanya la kuamka asubuhi, (iv) *B*, kwa kuelewa kuwa ni sentensi ya pili kwa sababu hufuata baada ya sentensi ya (ii) ambayo mara baada ya kuamka mwanafunzi anatakiwa kupiga mswaki na kwenda kuoga. Aidha, alipata sentensi ya (v) kwa kuandika *C* kwa sababu alielewa kuwa sentensi hiyo hufuata baada ya sentensi ya (iv) kwa sababu sentensi hiyo ina mwendelezo wa matukio kuwa mtu hupewa chai na chapati baada ya kuoga na kupiga mswaki.

Hata hivyo, alishindwa kipengele (iii) *D*, na (vi) *E* kwa kuwa alidhani kuwa mwanafunzi anaenda shule kwanza halafu anakunywa chai na

chapati ilihali mpangilio huo hauna mantiki. Kielelezo Na. 2.4.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama za wastani.

4. Sentensi zifuatazo zimechanganywa. Zipange katika mtiririko unaoleta maana kwa kuzipa herufi A, B, C, D na E. Sentensi ya (i) imetumika kama mfano.

(i) Nikifika shuleni ninaanza masomo. **E**

(ii) Kila siku ninaamka asubuhi. A

(iii) Kisha ninaondoka kwenda shuleni. D

(iv) Ninapiga mswaki na kuoga. B

(v) Dada ananipa chai na chapati. C

(vi) Ninakunywa chai kwa chapati. E

Kielelezo Na. 2.4.2: *Sampuli ya jibu la wastani katika swali la 4*

Kielelezo Na. 2.4.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi vipengele 3 na kushindwa vipengele 2 hivyo kupata alama za wastani.

Aidha, wanafunzi 671,449 sawa na asilimia 39.44 walipata kiwango hafifu kuanzia alama 0 hadi 2.5 kwani waliweza kujibu kipengele 1 tu au kushindwa kabisa. Hii inaonesha kuwa wanafunzi hao hawakuwa na umahiri wa kupanga sentensi katika mtiririko unaoleta maana. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alikosa vipengele vyote vitano kwani alishindwa kupanga msuko wa matukio kuanzia tukio la kwanza hadi la mwisho kwa kuhusianisha na maana katika sentensi za vipengele husika. Kielelezo Na. 2.4.3 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi ambaye alijibu vibaya swali hili.

4. Sentensi zifuatazo zimechanganywa. Zipange katika mtiririko unaoleta maana kwa kuzipa herufi A, B, C, D na E. Sentensi ya (i) imetumika kama mfano.

(i) Nikifika shuleni ninaanza masomo. **E**

(ii) Kila siku ninaamka asubuhi. B

(iii) Kisha ninaondoka kwenda shuleni. C

(iv) Ninapiga mswaki na kuoga. A

(v) Dada ananipa chai na chapati. D

(vi) Ninakunywa chai kwa chapati. E

Kielelezo Na. 2.4.3: *Sampuli ya jibu baya katika swali la 4*

Kielelezo Na. 2.4.3 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kupanga sentensi katika mtiririko unaoleta maana kutokana na kukosa umahiri wa kuunda kifungu cha habari hususani katika kuhusianisha matukio katika vipengele husika.

## 2.5 Sehemu E:

Sehemu hii ilikuwa na swali moja lenye vipengele vitano (5) vyenye jumla ya alama 10. Swali lilitoka katika umahiri wa *Kuonesha Uelewa wa Jambo Alilolisikiliza au Kulisoma*. Swali lilipima umahiri wa mwanafunzi wa kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali yaliyofuata.

**Swali la 5:** Soma kwa makini kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata kwa **kuandika jibu lililo sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi.

*Yoya na Bura wanaishi katika kijiji cha Ulanga. Watoto hao walikuwa na tabia ya ukaidi. Kila walipoonywa na wazazi wao hawakutii. Walimu pia walitimiza wajibu wao wa malezi hivyo mara kwa mara waliwashauri kuacha tabia ya ukaidi.*

*Japokuwa walionywa na walimu pamoja na wazazi lakini hawakubadilika.*

*Walipofika Darasa la Nne, watoto hao walianza tabia ya utoro na hatimaye waliacha shule. Walikubaliana kuanza biashara ya kuuza mkaa. Kila siku walikwenda msituni kukata miti kwa ajili ya kuchoma mkaa. Wazazi wao waliwaonya kwa kuwakumbusha katazo la serikali kuhusu ukataji wa miti ovyo.*

*Siku moja walipokwenda kukata miti msituni, viongozi wa serikali ya kijiji waliwavizia na kuwakamata. Walipelekwa kwenye ofisi ya kijiji. Huko walipata adhabu kali na kuamriwa kupanda miti ishirini kwa kila mmoja. Walijutia ukaidi wao na kuomba radhi kwa wazazi na walimu wao. Walisamehewa na walirudi shuleni kuendelea na masomo. Toka wakati huo watoto hao walikuwa na heshima na watiifu sana.*

**Maswali**

(a) Ni tabia zipi mbaya walizokuwa nazo Yoya na Bura?

(i) ____________________________________________

(ii) ____________________________________________

(b) Ni tabia gani iliwafanya Yoya na Bura kuacha shule?

____________________________________________

(c) Baada ya kupewa adhabu Yoya na Bura walifanya nini?


____________________________________________

(d) Habari hii inahusu nini? ______________________________

(e) Habari hii inakufundisha nini? ___________________________

____________________________________________

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuonesha Uelewa wa Jambo Alilolisikiliza au Kulisoma*. Swali lilijibiwa na wanafunzi 1,702,640 sawa na asilimia 100. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa cha wastani kwani wanafunzi 871,032 sawa na asilimia 51.2 ndio waliofanya vizuri. Wanafunzi 47,086 sawa na asilimia 2.77 waliweza kujibu vizuri sana vipengele vyote 5 na kupata alama 10. Aidha, wanafunzi 198,381 sawa na asilimia 11.65 walifanya vizuri na kupata alama 6.5 hadi 9.5. Wanafunzi 625,565 sawa na asilimia 36.74 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Vilevile, wanafunzi 831,608 sawa na asilimia 48.84 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 2.5. **Chati Na. 5** inaonesha viwango vya ufaulu vya wanafunzi kwa asilimia.




**Chati Na. 5**: *Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi katika swali la 5*

Uchambuzi unaonesha kuwa, wanafunzi 47,086 sawa na asilimia 2.77 walifaulu kwa kiwango kizuri sana. Wanafunzi hao waliweza kujibu kwa usahihi vipengele vyote 5 na kupata alama 10 kwani walikuwa na umahiri wa kusoma habari na kubaini mawazo yaliyomo ndani yake.

Kwa mfano, katika kipengele cha (a) kilichomtaka mwanafunzi aeleze tabia mbili mbaya walizokuwa nazo Yoya na Bura, alitoa jibu sahihi kuwa ni *tabia ya ukaidi na tabia ya utoro*. Vilevile, katika kipengele (d) kilichomtaka mwanafunzi kueleza habari inahusu nini, alitoa jibu sahihi kuwa habari *inahusu tabia ya Yoya na Bura.*

Aidha, katika kipengele cha (e) kilichomtaka mwanafunzi kueleza habari inafundisha nini, alitoa jibu sahihi kuwa ‘habari *inafundisha tuwe na nidhamu kwa wazazi wetu hata walimu.* Hii inadhihirisha kuwa, mwanafunzi huyo aliweza kusoma na kuelewa yaliyomo ndani ya kifungu cha habari. Kwa ujumla, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa wanafunzi wengi walikuwa na umahiri wa kusoma na kuchanganua mawazo yaliyomo kwenye kifungu cha habari. Kielelezo Na. 2.5.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu maswali kwa usahihi kutokana na habari aliyoisoma.

(a) Ni tabia zipi mbaya walizokuwa nazo Yoya na Bura?

(i) Tabia ya ukaidi.

(ii) Tabia ya utoro.

(b) Ni tabia gani iliwafanya Yoya na Bura kuacha shule?

Tabia ya utoro.

(c) Baada ya kupewa adhabu Yoya na Bura walifanya nini?

Waliomba radhi kwa wazazi na walimu wao.

(d) Habari hii inahusu nini? Tabia ya Yoya na Bura.


(e) Habari hii inakufundisha nini? Habari hii inatufundisha tuwe na nidhamu kwa wazazi wetu hata walimu.

Kielelezo Na. 2.5.1: *Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 5*

Kielelezo Na. 2.5.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu vizuri vipengele vyote 5 kutokana na kuwa na umahiri wa kusoma na kufahamu yaliyomo ndani ya habari.

Hata hivyo, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi 625,565 sawa na asilimia 36.74 walipata alama za wastani kuanzia 3 hadi 6. Wanafunzi hao waliweza kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa vipengele vingine. Mathalani, waliweza kujibu vipengele 2 hadi 3 vya swali. Aidha, walishindwa kujibu vipengele vingine kutokana na kukosa umahiri wa kusoma na kubaini mawazo yaliyomo katika habari husika. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alishindwa kujibu kipengele cha (a) (ii) kilichomtaka aeleze tabia mbaya walizokuwa nazo Yoya na Bura na kuandika *kukata miti ovyo* badala ya “utoro”.

Vilevile, katika kipengele (c) kilichomtaka aelezee Bura na Yoya walifanya nini baada ya kupewa adhabu, mwanafunzi huyo aliandika kuwa *Yoya na Bura walibadilisha tabia zao* badala ya "waliomba msamaha kwa wazazi na walimu". Kwa ujumla, mwanafunzi huyo hakuelewa kabisa maudhui yaliyomo katika habari husika. Kielelezo 2.5.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kujibu baadhi ya vipengele kwa usahihi.



**Maswali**

(a) Ni tabia zipi mbaya walizokuwa nazo Yoya na Bura?

(i) Ukaidi.

(ii) Kukata miti ovyo.

(b) Ni tabia gani iliwafanya Yoya na Bura kuacha shule?

Tabia ya utoro.

(c) Baada ya kupewa adhabu Yoya na Bura walifanya nini?

Yoya na Bura walibadilisha tabia zao. na


(d) Habari hii inahusu nini? Habari hii inahusu tabia mbay za wakina Bura na Yoya.

(e) Habari hii inakufundisha nini? Habari hii inanifundisha kuacha tabia mbaya.

*Kielelezo Na. 2.5.2: Sampuli ya jibu la wastani katika swali la 5*

Kielelezo Na. 2.5.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa vingine kwa sababu ya kukosa umahiri wa kutosha wa kusoma na kubaini yaliyomo katika habari.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 831,608 sawa na asilimia 48.84 walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwani walipata alama kuanzia 0 hadi 2.5. Wanafunzi hao, hawakuwa na umahiri wa kusoma na kuwasilisha mawazo yaliyotolewa katika habari. Baadhi yao walishindwa kujibu kwa usahihi kutokana na kutokujua kusoma na kuandika. Uchambuzi unaonesha kuwa wengine hawakuelewa kabisa maudhui ya habari husika. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alitoa majibu ambayo baadhi alinakili kutoka kwenye habari na mengine alibuni kwani hayakuwa na uhusiano na matakwa ya swali. Hivyo, kupata kipengele kimoja tu (b) na kukosa vipengele (a), (c), (d) na (e). Kielelezo Na. 2.5.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.


**Maswali**

(a) Ni tabia zipi mbaya walizokuwa nazo Yoya na Bura?

(i) Watoto walikuwa Shuleni

(ii) wanafunzi wanapenda kucheza

(b) Ni tabia gani iliwafanya Yoya na Bura kuacha shule?

Utoto

(c) Baada ya kupewa adhabu Yoya na Bura walifanya nini?

adhabu wa kuchota maji

(d) Habari hii inahusu nini? inahusu wanafunzi shule

(e) Habari hii inakufundisha nini? Walimu

Utoto wazazi wao

Kielelezo Na. 2.5.3: *Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 5.*

Kielelezo Na. 2.5.3 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyejibu vibaya kutokana na kukosa umahiri wa kusoma na kuwasilisha mawazo yaliyotolewa katika habari kwa usahihi.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI

Upimaji wa somo la Kiswahili umehusisha umahiri wa *Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali* na *Kuonesha Uelewa wa Jambo Alilosikiliza au Kulisoma.* Aidha, wanafunzi walipimwa uwezo wa kusikiliza na kuandika matamshi ya silabi, maneno na sentensi (Imla), umahiri wa kutambua nyakati mbalimbali, kutoa maana ya nahau na kukamilisha methali mbalimbali, kupanga sentensi katika mtiririko unaoleta maana pamoja na umahiri wa kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika habari.

Uchambuzi wa viwango vya ufaulu kwa maswali unaonesha kuwa, kuna maswali yaliyokuwa na ufaulu wa kiwango kizuri sana, kizuri, na wastani. Swali la 1 ambalo lilipima umahiri wa mwanafunzi wa kusikiliza matamshi ya silabi, maneno na sentensi (Imla), lilikuwa na asilimia 85.1 ya ufaulu. Swali la 2 lililopima umahiri wa kutambua nyakati mbalimbali lilikuwa na ufaulu wa asilimia 85.7. Aidha, swali la 3, ambalo lilipima umahiri wa kutoa maana ya nahau na kukamilisha methali mbalimbali lilikuwa na ufaulu wa asilimia 69.6. Vilevile, Swali la 4, lililotoka katika umahiri wa kupanga sentensi katika mtiririko unaoleta maana lilikuwa na ufaulu wa asilimia 60.6 na Swali la 5, lililopima umahiri wa kusoma na kuchanganua mawazo yaliyopo katika habari, lilikuwa na asilimia 51.2 ya ufaulu.

Aidha, kati ya maswali yote, swali la 2 lilikuwa na kiwango kizuri zaidi cha ufaulu kwa asilimia 85.7, ilihali swali la 5 lilikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa asilimia 51.2. Hata hivyo, umahiri wa Kuwasiliana katika Miktadha Mbalimbali ndio uliokuwa na kiwango cha juu cha ufaulu kwa asilimia 77.13 ikilinganishwa na umahiri wa

Kuonesha Uelewa wa Jambo Alilosikiliza au Kulisoma ambao ulikuwa na ufaulu wa asilimia 60.40.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa viwango vya ufaulu katika vipengele vya umahiri vilivyopimwa unaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu kwa vipengele vyote 2 katika mwaka 2020 ni kizuri ingawa kuna kushuka kwa asilimia 1.56 ikilinganishwa na mwaka 2019. Kiwango cha ufaulu kwa mwaka 2019 kilikuwa asilimia 72.00 lakini mwaka 2020 kilikuwa asilimia 70.44. Vilevile, uchambuzi huu umebaini changamoto mbalimbali zilizosababisha wanafunzi kushindwa kujibu baadhi ya maswali kwa usahihi. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na kushindwa kuelewa matakwa ya swali, kushindwa kuelewa na kuchambua mawazo yaliyopo katika kifungu cha habari. Vilevile, uwepo wa athari ya lugha mama pamoja na kushindwa kumudu stadi za kusoma na kuandika zilikuwa kati ya changamoto zilizojitokeza. Pia, kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana za nahau pamoja na kukamilisha methali mbalimbali. Aidha, changamoto nyingine ni kushindwa kupanga sentensi katika mtiririko unaoleta mantiki kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uandishi wa habari fupi hususani katika kupanga mawazo kwa mtiririko unaoleta mantiki ili kuunda kifungu cha habari.

Ili kukabiliana na changamoto hizo ni vyema jitihada za makusudi zifanyike ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili, hivyo kuinua kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Mambo yafuatayo hayana budi kuzingatiwa ili kuinua kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne;

(a) Walimu watilie mkazo ufundishaji wa kusikiliza na kuandika imla, kwa kufanya yafuatayo;

   (i) Kuhakikisha wanafunzi wanaweza kutamka na kuandika sauti za herufi mwambatano mfano *gh, py, pw, sw, nyw* na nyingine katika silabi. Walimu pia watilie mkazo matamshi ya maneno na sentensi kwa usahihi kwa kuwapa wanafunzi mazoezi ya mara kwa mara wakiwa katika vikundi.

   (ii) Kuwapa wanafunzi mazoezi ya mara kwa mara ya kutamka na kuandika kwa usahihi maneno yenye herufi ‘s’ na ‘th’ pamoja na ‘z’ na ‘dh’ katika silabi, neno na sentensi kwa kutumia mbinu ya bungua bongo na kutumia picha mbalimbali.

(b) Walimu watilie mkazo ufundishaji wa nyakati mbalimbali katika vitenzi kwa kuwaweka wanafunzi katika vikundi ili wajadili kuhusu nyakati mbalimbali. Walimu watumie picha au chati zinazoonesha viambishi vya wakati katika vitenzi kama vile; kiambishi -na- kuonesha wakati uliopo, -ta- kuonesha wakati ujao, -li- kuonesha wakati uliopita na -me- kuonesha wakati timilifu.

(c) Walimu watilie mkazo ufundishaji wa nahau na methali hasa katika kutoa maana ya nahau na miundo ya methali kwa kuwaweka wanafunzi katika vikundi na kutumia picha mbalimbali kujadili methali. Aidha, wanafunzi wapewe mazoezi ya

kukusanya nahau na methali mbalimbali na kutafuta maana zake kwa kutumia mbinu ya kazi mradi.

(d) Walimu wanatakiwa kuweka msisitizo katika ufundishaji wa utungaji wa habari fupi hususan kupanga mawazo yenye mtiririko unaoleta mantiki. Ili kufanikisha hili, mbinu za ujifunzaji zifuatazo hazina budi kuzingatiwa;

(i) Wanafunzi wakae katika vikundi wajadili na wapange mawazo hayo kimantiki ili wapate habari kamili.

(ii) Wanafunzi waelezee katika vikundi jinsi walivyo panga mawazo kimantiki na kupata habari kamili.

(e) Walimu watilie mkazo katika ufundishaji wa kusoma habari fupi katika vikundi na kubaini maudhui yaliyomo kwa kutumia matini mbalimbali ili kuwajengea uwezo wa kufanya uchambuzi makini katika habari.

**KIAMBATISHO A**

## ULINGANIFU WA UFAULU KWA WANAFUNZI KWA KILA UMAHIRI KATIKA SFNA 2019 NA SFNA 2020

| Na. | Umahiri Mkuu | Upimaji 2020 | | | | Upimaji 2019 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | |
| 1. | Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1 | 85.1 | 77.13 | Vizuri | 1 | 86.7 | 76.8 | vizuri |
| | | 2 | 85.7 | | | 3 | 69.8 | | |
| | | 4 | 60.6 | | | 4 | 73.9 | | |
| 2. | Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma | 3 | 69.6 | 60.40 | Wastani | 2 | 59.9 | 64.6 | Wastani |
| | | 5 | 51.2 | | | 5 | 69.3 | | |

CMYK-